Habari Leo, Jumatatu Agosti 25, 2025



YA ZIWA

imiyu, Mara, Kagera

# Madereva bodaboda wakumbushwa kuzingatia sheria za barabarani

Na Kareny Masasy, Shinyanga

WAENDESHA pikipiki maarufu bodaboda mkoani Shinyanga wametakiwa kuendelea kuzingatia sheria za usalama barabarani, hasa kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi mkuu ambapo mikusanyiko ya watu itakuwa mingi takribani kila sehemu.

Ofisa usalama barabarani mkoa, Emmanuel Mwaitaga alisema juzi katika kikao cha bodaboda kwamba miongoni mwa mambo yanayosisitizwa ni kuacha utamaduni wa kupakia abiria zaidi ya mmoja, ili kuepuka ajali.

"Na sheria ya usalama barabarani inamtaka dereva kupata mafunzo ya udereva, kisha anapewa leseni ya daraja 'A' kabla ya kuanza kuendesha chombo cha moto," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Usalama barabarani mkoa, Fraterimi Tesha alikemea baadhi ya bodaboda wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu badala ya kufanya kazi iliyolengwa.

"Tunawataka wabadili tabia na kuwa raia wema," alisema.

Naye Mratibu wa Mfunzo ya muda mfupi Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) mkoa, Yona Mwambopa alisisitiza suala la bodaboda kupata mafunzo ya udereva kabla ya kuingia barabarani na kuongeza kuwa gharama za kupata ujuzi huo zimekuwa zikipunguzwa ili kuwafikia vijana wengi.

Siku za kujifunza pia zimekuwa zikipunguzwa, ambapo hivi karibuni kumekuwepo na kampeni ya uhamasishaji iliyohusisha punguzo la gharama kutoka kutoka Sh 50,000 kwa wiki mbili, hadi Sh 35,000 kwa siku tano.

"Hata hivyo, bado mwitikio ulikuwa chini kwani walijitokeza watu 35 tu. Tunaendelea kuhamasisha ili waje wengi kupitia viongozi wa vikundi vyao," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa waendesha bodaboda Wilaya ya Shinyanga, Mohamed Mlabbu alisema suala la madereva kutii sheria bila shuruti ni moja ya vipaumbele, ikizingatiwa kwamba kipindi cha kampeni bodaboda wengi huwa wanachukuliwa na vyama vya siasa kwa ajili ya kusherehesha.



Mraghibishi kutoka Shirika la Twaweza, Richard Temu akiwasilisha mada wakati wa mafunzo kuwajengea uwezo waraghibishi kutoka katika vijiji wilayani Maswa Mkoani Simiyu (Picha na Derick Milton).

# Polisi, Latra yawabana madereva wanaopindisha sheria

Na Yohana Shida, Geita

JESHI la Polisi mkoani Geita kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) limeanza msako wa waendeshaji pikipiki za magurudumu matatu maarufu bajaji wasiozingatia sheria za barabarani.

Mkuu wa Usalama barabarani mkoa, Aloyce Jacob alilieleza HabariLEO juzi kwamba, "Hatua hiyo inatokana na ongezeko la bajaji, huku madereva wakibainika kuwa kiini cha ongezeko la ajali kutokana na kukiuka sheria za barabarani," alisema.

Aliongeza: "Bajaji kawaida inapaswa kubeba abiria watatu lakini inapakia zaidi ya uwezo wake. Kadhalika dereva anapaswa kuwa na leseni, awe amepitia mafunzo ya udereva. Wanaovunja sheria hizi tutawachukulia hatua stahiki, ikiwemo kuwapeleka mahakamani".

Alisisitiza kwamba oparesheni hiyo imelenga kuimarisha usalama wa dereva, abiria na watumiaji wengine wa barabara.

"Unakuta bajaji inapakia abiria mpaka eneo la dereva na kusababisha ashindwe kumudu usukani ipasavyo, na kusababisha ajali kizembe. Tuko macho kuhakikisha ajali za makusudi zinadhibitiwa," alisema. Kwa upande wake, Ofisa Leseni Latra Mkoa, Kenani Katindasa alisema operesheni hiyo ni endelevu ili kukomesha tabia ya madereva kufanya kazi kwa mazoea, ikiwa ni pamoja na kuendesha vyombo vya moto bila leseni.

Wakati huo huo, aliwashauri wananchi kutoshawishika kupanda vyombo vya usafiri vinavyovunja sheria, kwani wanajiweka katika hatari kiasi cha kuweza hata kupoteza maisha ama kupata ulemavu wa kudumu.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Madereva Bajaji mkoa, Mussa Kisoke aliahidi kutoa ushirikiano kwa jeshi la polisi ili kudhibiti ajali zinazotokana na uvunjifu wa makusudi wa sheria za usalama barabarani.

Alisema mpaka sasa mkoa wote una takribani leseni 2,600 za bajaji, wakati leseni 1,500 zikiwa zimesajiliwa katika Mji wa Geita pekee.

CamScanner

The Guardian, Monday August 25, 2025 Pg 1



Staff apparently with Dar es Salaam's Bus Rapid Transit (BRT) network pictured yesterday blocking one of the firm's buses from moving, after the saloon car (R) allegedly "invaded" their lane near the Shekilango junction of Morogoro Road. Photo: Correspondent Imani Nathaniel

# HABARI KITAIFA



Wahudumu wa basi la Mwendokasi wakiwa wamesimama mbele ya gari wakigoma kuendelea na safari baada ya gari dogo (kulia) kudaiwa kuingilia barabara sehemu ya kuvukia katika barabara ya Morogoro eneo la Shekilango, Dar es Salaam jana. **PICHA IMANI NATHANIEL**

Zanzibar Leo



KERO




***MAKONDA wa Dala dala wakikataa kupakia abiria katika kituo cha dala dala Kisonge wakati kituo hicho kikiwa kimepewa amri ya kupakia na Serikali ya Mkoa wa Mjini Magharibi.***

UCHAMBUZI



Daladala zikipita Barabara ya Uhuru, Ilala mkoani Dar es Salaam bila kuheshimu sheria za barabarani hali inayosababisha usumbufu zinapokutana na magari mengine ambayo yako kwenye njia sahihi. (Picha na Rahel Pallangyo).

Habari Leo Pg 17
Jumatatu Agosti 25, 2025

CamScanner



Motorcycle taxi riders queue to make road toll payments at a Kigamboni Bridge point in Dar es Salaam yesterday when heading to the city centre, a situation widely condemned as time-wasting. Photo: Correspondent Sabato Kasika

The Guardian Monday 25, August 2025 Pg6